



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA.

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza utafanyika Mkao wa Kigoma tarehe 01 Julai, 2024. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Mara baada ya uzinduzi, zoezi la uboreshaji wa Daftari litaendelea Mkoani Kigoma hadi tarehe 07 Julai, 2024.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumatatu tarehe 01 Julai, 2024 hadi siku Jumapili tarehe 07 Julai, 2024
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivymo katika Mitaa, vijji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

Uboreshaji utahusisha: -


1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura amba kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha, Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuwanu ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

MAMBO YA KUZINGATIA

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahu wapiga kura amba waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA

Limetolewa leo tarehe 01/06/2024 na:


Kailima, R. K
MKURUGENZI WA UCHAGUZI